BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA KUMI NA MOJA

Kikao cha Ishirini na Tatu – Tarehe 09 Juni, 2023

Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

## I. MASWALI:

### Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:

180. MHESHIMIWA BAKAR HAMAD BAKAR (Jimbo la Wawi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, uratibu na Baraza la Wawakilishi:

Katika kuhakikisha Wawakilishi wa wananchi wanakuwa karibu na wananchi wao, kuna haja kubwa ya kuwepo kwa ofisi zao katika majimbo yao.

Je, Serikali haioni kuwa ipo haja ya kujenga ofisi za Wawakilishi majimboni mwa Wawakilishi hao.

### Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

165. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

(a) Je, ni kwa kiasi gani elimu inayotokana na athari ya taka sumu za kieletroniki inatolewa na kuwafikia wananchi.

(b) Taka hizi zina athari gani kiafya na kimazingira katika maeneo tunayoishi.

(c) Ni mkakati gani wa makusudi Serikali itautumia katika

kuzitokomeza/kuziondosha kabisa taka hizi zenye sumu za kieletroniki hususan kwenye mlundikano wa majaa mbali mbali katika mji wetu.

<u>Wizara ya Afya:</u>

45. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Tunaipongeza Serikali kwa kuimarisha miradi ya ujenzi wa hospitali kubwa za kisasa za Wilaya kwa lengo la kuwapatia huduma bora wananachi wake.

(a) Kutokana na uhaba mkubwa wa madaktari bingwa, Je, Wizara ya Afya imejipanga vipi kuhakikisha inatatua changamoto ya uhaba huo.

(b) Je, huduma ya Bima ya Afya itapatikana katika hospitali mpya za Wilaya.

<u>Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:</u>

141. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi:

Katika msimu huu wa mvua unaoendelea barabara nyingi sana zimeharibika na zimekuwa na mashimo ambayo yanaweza kusababisha ajali barabarani.

Je, Serikali ina mpango gani wa dharura wa kuzihami barabara hizo.

<u>Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda</u>:

155. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Miongoni mwa mabadiliko yaliyoletwa na viwanda hapa nchini mwetu, ni kupunguza utamaduni wetu wa kutengeneza juisi za asili za kutumia matunda tulizozizoea kutengenezwa majumbani mwetu kutokana na kuongezeka kwa kasi kubwa ya juisi za viwandani. Hata hivyo, kuna malalamiko ya usalama wa afya juu ya juisi hizi zinazotengenezwa viwandani.

(a) Je, ni mchanganyiko wa kemikali ngapi za kutunzia kitaalamu zinazotumiwa katika juisi mbali mbali za

viwandani ambazo hatimae hufikishwa madukani kwa lengo la kutumiwa na mlaji.

(b) Ni yepi madhara ya kutumia mchanganyiko wa kemikali nyingi za kutunzia juisi hizi za madukani kwa afya ya mlaji.

**Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi:**

229. MHESHIMIWA PROF. OMAR FAKIH HAMAD (Jimbo la Pandani) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchumi wa Buluu na Uvuvi:

Katika utaratibu wa sasa, Serikali haijakuwa na mbinu madhubuti ya kuhakikisha kwamba maliasili za Zanzibar zinawanufaisha watu wote kwa usawa.

(a) Je, kwa kiasi gani leseni za utalii wa bahari (Sport fishing) zikiwemo zile za Kisiwa cha Latham na za Mawakala wa Utalii (Tour Operators) zinakidhi sifa za kimataifa.

(b) Je, ni migogoro mingapi ya mipaka na matumizi baina ya wavuvi kwa wavuvi na baina ya wavuvi na watalii wa baharini na Serikali, haijapatiwa ufumbuzi na iko katika hatua gani.

(c) Kwa kuwa kuna ukiukwaji wa sheria uliofanyika katika baadhi ya mikataba na makubaliano ya kuruhusu wageni wa nje kuingia katika maeneo nyeti kama ya Mnemba, Latham Island na Misali, Je, Serikali iko katika hatua gani ya kuzirekebisha kasoro hizo.

**Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali:**

244. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:

Kwa kuwa Zanzibar ina uwanja wa ndege wa Kimataifa (Karume International Airport) na tayari Serikali imeshadhamiria kujenga uwanja mwengine mkubwa wa kimataifa kisiwani Pemba. Na kwa kuwa, kujengwa na kuimarishwa kwa viwanja hivi kutasababisha ongezeko kubwa la ndege za ndani na nje ya nchi mbali mbali. Na kwa kuwa ongezeko hilo linaweza kusababisha msongomano mkubwa wa ndege zinazotaka kuruka pamoja na zile zinazohitaji kutua kwa wakati mmoja. Na kwa kuwa jambo hili linahitaji utaalamu mkubwa katika kulidhibiti huku tukiwa na upungufu mkubwa wa utaalamu huo.

Je, ni lini Serikali kupitia Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA) itaanzisha kitivo cha ‘Airport Craft Control and Piloting’ ili kuondosha mapungu hayo.

**Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:**

158. MHESHIMIWA AMEIR ABDALLA AMEIR (Jimbo la Mwanakwerekwe) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Iliyokuwa Wizara kabla ya Wizara hii ya Utalii na Mambo ya Kale, ilikuwa na dira na dhamira inayoendana na Wizara hiyo.

Je, kwa sasa Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale inaendeshwa kwa dira na dhamira ipi.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**Waziri wa Maji, Nishati na Madini:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maji, Nishati na Madini kwa mwaka 2023/2024.

Zanzibar,
09 Juni, 2023.

(Raya Issa Msellem)
KATIBU WA BARAZA